HAYDOM INSTITUTE OF HEALTH SCIENCES
ELCT Mbulu Diocese

FOMU YA KUJIUNGA NA TAASISI YA MAFUNZO YA SAYANSI ZA AFYA HAYDOM KWA MWAKA WA MASOMO 2018/2019

Ndugu
…….

Ninakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Taasisi ya Mafunzo ya Sayansi za afya Haydom. Ninakutaarifu kuwa wewe umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya **UGANGA** kwa Ngazi ya stashahada (Diploma in clinical medicine) kwa mwaka wa masomo 2018/2019.

Taasisi hii ina jumla ya vitengo vitatu kama ifuatavyo.

1. Kitengo cha Uuguzi
2. Kitengo cha Maafisa Tabibu.
3. Kitengo cha Wateknolojia wa Maabara.

Masomo yataanza tarehe 15.10.2018 siku ya Jumatatu

1. 0. Geografia.

Taasisi ipo katika Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Mbulu, Tarafa ya Haydom na Kata ya Haydom.

Taasisi ipo umbali wa kilomita 300 kusini Magharibi mwa Jiji la Arusha na Kilometa 122.4 kaskazini Magharibi mwa mji wa Babati. Taasisi ipo ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Kilutheri Haydom ambapo wanafunzi wetu hufanya mazoezi ya vitendo. Hospitali ina wataalamu wa fani mbalimbali, vifaa vya kutosha kwa mazoezi ya vitendo. Taasisi ina uzoefu wa miaka 36 katika fani ya Uuguzi, na miaka miwili kwa fani za Maafisa Tabibu na Mafundi Sanifu wa Maabara. Taasisi imesajiliwa na NACTE kwa usajili nambari **HAS/006/2002** na imepata ithibati (full accreditation) ya NACTE na inayo waalimu wa kutosha na wenye uzoefu wa kufundisha taaluma katika fani za afya.

HAYDOM INSTITUTE OF HEALTH SCIENCE
ELCT Mbulu Diocese

2. 0. MSINGI WA TAASISI YA MAFUNZO YA SAYANSI ZA AFYA HAYDOM.

Taasisi ya Mafunzo ya Sayansi za Afya Haydom inamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mbulu.

2.1. Msingi wa kwanza ni wa Kikristo, Taasisi kinafuata misingi ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mbulu.

3.0. Msingi wa pili ni wa siasa ya kujitegemea **(Self-reliance)** hivyo Taasisi ina miradi ya kilimo cha mbogamboga, miti ya matunda na ufugaji wa nguruwe. Wanafunzi **wote** wanawajibika katika utunzaji wa miradi hiyo, kwa mujibu wa sheria za taasisi ni lazima kila mwanafunzi kushiriki katika miradi hiyo.

4. 0 ADA NA MICHANGO MBALIMBALI

FEE STRUCTURE 2018/2019
CLINICAL MEDICINE DEPARTMENT
DIPLOMA

DESCRIPTION	NTA LEVEL 4		NTA LEVEL 5		NTA LEVEL 6	
	FIRST SEMESTER	SECOND SEMESTER	THIRD SEMESTER	FOURTH SEMESTER	FIFTH SEMESTER	SIXTH SEMESTER
Tuition fee	600,000.00	600,000.00	600,000.00	600,000.00	600,000.00	600,000.00
Accomodation	200,000.00	200,000.00	200,000.00	200,000.00	200,000.00	200,000.00
Meal	320,000.00	320,000.00	320,000.00	320,000.00	320,000.00	320,000.00
Registration fee	10,000.00	-	-	-	-	-
NHIF	50,400.00	-	50,400.00	-	50,400.00	-
NACTE	15,000.00	-	15,000.00	-	15,000.00	-
National Exam fee direct to Ministry	150,000.00	-	150,000.00		150,000.00	
Research fee	--	-	-	-	-	50,000.00
Rehabilitation	50,000.00	-	-	-	-	-
Community field	-	-	150,000.00		150,000.00	-
Caution money	10,000.00	-	-	-	-	-
Sports	10,000.00	-		-		-
Uniforms	100,000.00	-	-	-	-	-
Clinical Coat	80,000.00	-	-	-		-
Reagents and Medical Equipment (Teaching lab)	50,000.00	-	50,000.00	-	-	-
Supervision fee for CSSC/diocese	8,000.00	-	8,000.00	-	8,000.00	-
Students union	2,500.00	-	2,500.00	-	2,500.00	-
Practical hospital fee HLH	10,000.00	-	10,000.00	-	10,000.00	-
Identity card	5,000.00	-	-	-	-	-
Graduation Gown	-	-	-	-	-	30,000.00
Graduation - finalist	-	-	-	-	-	20,000.00
TOTAL FOR SEMESTER	**1,670,900**	**1,120,000**	**1,555,900**	**1,120,000**	**1,505,900**	**1,220,000**
ANNUAL FEE	**2,790,900**		**2,675,900**		**2,725,900**	

4.1 JINSI YA KULIPA

Kwa Watanzania, siku ya kuja kuanza masomo mwanafunzi aje na ada yote ya muhula wa kwanza kama inavyoonekana kwenye jedwali la ada la darasa husika,na utalipa kwa utaratibu ufuatao:

4.1.1 Ada ya malazi (Accommodation fee) italipwa kwenye akaunti ya taasisi ya CRDB

JINA LA AKAUNTI: HAYDOM INSTITUTE OF HEALTH SCIENCES
NAMBA YA AKAUNTI: **0150271030300**
BENKI: CRDB
TAWI: HAYDOM

4.1.2 ADA YA MASOMO NA MICHANGO MINGINE ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA TAASISI YA CRDB TU.

JINA LA AKAUNTI: HAYDOM INSTITUTE OF HEALTH SCIENCES
NAMBA YA AKAUNTI: **0150271030301**
BENKI: CRDB
TAWI: HAYDOM
Au

NMB
JINA LA AKAUNTI: HAYDOM SCHOOL OF NURSING
NAMBA YA AKAUNTI: **41210004975**
BENKI: NMB
TAWI: DAR ES SALAAM

4.1.3 ADA YA MTIHANI WA TAIFA.

NMB
JINA LA AKAUNTI: APPLICATION AND EXAMINATION ACCOUNT
NAMBA YA AKAUNTI: **20110007946**
BENKI: NMB TAWI: MBULU

Mwanafunzi anapaswa awe amemaliza kulipa fedha zote za ada ya muhula mmoja kabla ya kuanza muhula mwingine, vinginevyo hataruhusiwa kufanya mitihani ya mwisho wa muhula huo.

4.0 SHERIA ZA TAASISI KWA UJUMLA

4.1 Taasisi inafuata sheria zaWizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia taasisi imejiwekea sheria ndogo ndogo katika mazingira yake ambazo mwanafunzi anapaswa kuzifuata.

4.2 Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele, na wa kiume hawaruhusiwi kufuga ndevu

4.3 Mwanafunzi anaweza kushindwa kuendelea na masomo/kufukuzwa shule kwa sababu zifuatazo:

a) Akishindwa mitihani na ikiwa maendeleo yake hayaridhishi
b) Kushindwa/kutii sheria za taasisi ambazo atapewa na kutia saini pindi anapofika chuoni.
c) Kuonyesha tabia isiyoendana na maadili ya kazi za afya.
d) Kushindwa kulipa ada kwa wakati.
e) Sababu za kiafya ambazo zitamfanya asimudu masomo yake.

5. MITAALA

Taasisi inatumia mitaala ya mafunzo kutoka Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee naWatoto na uliyoidhishwa na NACTE.

6. VITU AMBAVYO MWANACHUO ANATAKIWA KUVILETA:

a. Birth certificate - original,
a) Vyeti halisi vya secondary (Original certificates)
b) Saa ya mkononi
c) BP machine, Stethoscope, Patella hammer, Tape measure, examination torch
d) Taulo 2, masweta mawili **MEUPE (masweta yenye kofia hayaruhusiwi kabisa)**
e) Shuka 4 na foronya 2 (shuka 2 pinki na blue bahari 2)
f) Ndoo 1
g) Squizer, hardbroom, softbroom
h) Ream 1 A4
i) Rulled paper 1 (karatasi za mistari)
j) Passport size 2
k) Madaftari, rula, Kalamu, penseli, na penseli za rangi (zina patikana chuoni)
l) Nguo za binafsi, Mavazi yote yawe ya heshima kumbuka Taasisi yetu ya Mafunzo ya Sayansi za Afya ni Taasisi ya Kanisa na ipo kijijini ambapo mavazi kama

suruali kwa wasichana, nguo fupi na zilizobana hazikubaliki katika jamii hii.

m) Viatu vyeusi vya ngozi jozi (pair) mbili vyenye visigino vifupi
n) Soksi jozi tatu na kuendelea.

7 SARE ZA TAASISI

Sare zilizokubaliwa na Wizara katika vyuo vya Afya ni:-

Mwanachuo atatakiwa kuvaa sare zitakazoshonwa hapa chuoni kufuatana na mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hii ni kulingana na taaluma husika unayosomea na jinsi itakavyoainishwa na mabaraza ya taaluma hizo.

8. UCHELEWAJI.

Tunakushauri uwahi siku ya kuanza shule, ukichelewa mtu mwingine atapewa nafasi yako baada ya wiki moja. Mwanafunzi atapata likizo ya wiki 4 kila mwaka na akichelewa baada ya likizo **atalipa siku alizochelewa mara mbili katika likizo inayofuata**.

Kama kuna sababu maalumu (isiwe karo) mzazi atume taarifa chuoni, na kama ni ugonjwa mwanafunzi aje na cheti cha Daktari.

9. MSIBA.

Ikiwa kwa bahati mbaya mwanafunzi atapata msiba, mzazi anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Taasisi na si mwanafunzi (mtoto wake) Mkuu wa Taasisi atamfahamisha mwanafunzi huyo aliyepata msiba. Mwanafunzi anaruhusiwa kwenda kwenye msiba wa watu wafuatao:-

a. Wazazi (Baba/Mama)
b. Kaka na Dada
c. Mtoto wake
d. Mume/Mke

KUWA SIFA YA UTUKUFU WAKE. (Ef 1;14b)



BARTHOLOMAYO MADANGI
MKUU WA TAASISI